

4. Lishe na virutubisho vinakuwa sehemu muhimu katika matibabu ya watoto waliozaliwa na mama mwenye VVU.
5. Dawa mbili au tatu zilizochanganywa za kupunguza makali ya VVU kwa ajili ya watoto zinapatikana katika ngazi zote za huduma ya afya.
6. Kuongeza wataalamu wa afya ambao wana uzoefu pamoja na kuruhusu watu wanaoishi na VVU wenye uzoefu na dawa kutoa huduma hospitalini zisizohitaji utaalumu mkubwa.

## JINSI YA KUSHIRIKI

Ili kushiriki au kujifunza zaidi kuhusu kampeni ya kutokomeza maambukizi VVU kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto wasiliana na;

**Idara ya Sera na Ushawishi,  
Human Development Trust (HDT),  
P.O.BOX 65147  
Dar Salaam**

**Email: [info@hdt.or.tz](mailto:info@hdt.or.tz) au [advocacy@hdt.or.tz](mailto:advocacy@hdt.or.tz)**



## KAMPENI YA KUTOKOMEZA MAAMBUKIZI YA VIRUSI VYA UKIMWI TOKA KWA MAMA KWENDA KWA MTOTO

### Utangulizi

***"...Tukiona watoto tunafikiria maisha yajayo. Tunafikiria ndoto za mafanikio yao kimaisha endapo watakuwa wakubwa...."*** Mkurugenzi Mtendaji wa HDT  
Dr Peter Bujari

Leo hii katika Tanzania kuna akina mama 118,000 wanaoishi na virusi vya UKIMWI kila mwaka, ambao wanawaambukiza watoto wao karibu 40,000 kila mwaka. Maambukizi haya ni sawa na watoto 118 wanaoambukizwa kila siku. Kama watoto hawa 40,000 wasipopata matibabu, nusu yao watapoteza maisha kabla ya umri wa miaka miwili. Kama matibabu yasipopatikana kwa watoto hawa, robo tatu watapoteza maisha kabla ya umri wa miaka mitano.

*.....Ukweli ni kwamba maambukizi haya yanaweza kuzuilika... tunaweza kuponya maisha ya watoto hawa kwa kuhakikisha kuwa akina mama wajawazito wote wenye VVU wanapima na kupata dawa ya kuzuia kumwambukiza mtoto (PMTCT).*



### Tatizo

Kwa wastani ni akina mama wajawazito wenye VVU 65 kati ya mia wanapata huduma ya PMTCT. Hata hivyo namba hiyo ni ndogo katika mikoa ya Tanga, Rukwa, Mwanza, Morogoro, Mara nk. Watoto ambao wanapata matibabu ya kuzuia wasiambukizwe na mama zao ni wanne kati ya kumi ikimaanisha kuwa sita kati ya kumi hawapati huduma. Kuna sababu nyingi zinazochangia hali hiyo ikiwa ni pamoja na:

- 1.0. Upungufu wa wafanya kazi wa afya kwa ajili ya kutoa huduma za PMTCT na zile za matibabu kwa watoto waliozaliwa kwa mama wenye VVU,



- 2.0. Kutoelewa ukubwa wa tatizo la watoto wanaohitaji dawa kuzuia wasiambikizwe na wanaohitaji dawa kwa ajili ya matibabu,
- 3.0. Kutopatikana kwa dawa zilizochanganywa kama za watu wazima na uhaba wa dawa za septrin kwa ajili ya kuzuia magonjwa nyemelezi na vipimo vingine,
- 4.0. Kuchelewa kwa wagonjwa kufika kwenye vituo au kutofika kabisa kwa sababu ya umbali, unyanyapaa na wakati mwingine mtazamo wa wafanyakazi wa afya,
- 5.0. Kukosekana kwa huduma mseto ambapo huduma zipo sehemu mbali mbali ikiwa ni pamoja na ushiriki wa wanaume kwenye afya ya uzazi. Pia ni vituo saba kati ya mia tu vinatoa huduma ya PMTCT kwenye ngazi ya zahanati,
- 6.0. Vipimo na fomu zinazotumika kwenye CTC kutozingatia mahitaji ya makuzi ya mtoto kwenye fomu za CTC -2,
- 7.0. Kutokuwepo kwa sera ya kutoa virutubisho kwa watoto waliozaliwa na mama mwenye VVU anaenyonyesha hali ambayo inasababisha watoto kupata utapiamlo au kuambukizwa VVU na mama zao wakati wa kunyonya,
- 8.0. Kutokuwepo kwa fedha za kutosha kugharimia mahitaji ya programu ya PMTCT katika ngazi zote.

### **CEPA itafanya Ushawishi na Utetezi kutimiza malengo yafuatayo;**

1. **Matunzo katika familia pamoja na lishe** – kupanua upatikanaji wa huduma za kuzuia maambukizi ya VVU kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto (PMTCT). Maeneo mengine yatakua, huduma mseto zinazopatikana pamoja ikijumuisha huduma za uzazi wa mpango, chanjo, lishe, septrine na ushiriki wa mme.
2. **Uchunguzi wa mapema na Tiba Sahihi kwa Watoto** - Kupanua upatikanaji wa uchunguzi mapema na tiba sahihi kwa watoto ili kupunguza vifo na kuongeza ubora wa afya zao.

3. **Upatikanaji wa tiba muafaka** – kupunguza vikwazo na kuongeza huduma za kiwango, dawa zenye ubora ila za bei rahisi ili kuokoa maisha ya watoto na familia zao, zikiwemo ARVs na dawa za kutibu magonjwa nyemelezi.
4. **Fedha za kutosha kupambana na maambukizi ya mama kwenda kwa mtoto** – kupata fedha za kutosha zinazohitajika ili kuwezesha utekelezaji wa mkakati wa kuzuia maambukizi ya VVU kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto (PMTCT), na miradi ya kitaifa ya kutibu watoto na mama wajawazito.

### **Mtandao wa kampeni ya CEPA**

Kampeni ya kutokomeza maambukizi ya VVU ina lengo la kuunga mkono jitihada za kitaifa za kuhakikisha hakuna mtoto anaambukizwa VVU kutoka kwa mama. Itahusisha vyama vya kiraia wataalamu na waandishi wa habari kutatua matatizo ya kijamii, kiuchumi, kimila na kidehuri pamoja na kisiasa. Hatimaye, CEPA itajenga mtandao wa ushawishi ambao utasaidia kuona ufuatiliaji na uwajibikaji wakati miradi ya kuzuia maambukizi na matibabu vinaongezewa uwezo katika nchi zote barani Afrika. Kwa kufanya hivyo, kampeni itaendelea kujenga uwezo wa kushawishi na uwajibikaji ambao unaweza kutekelezeka katika nchi nyingine na baadae kuigwa katika sehemu nyingine duniani.

### **Matokeo muhimu yanayotegemewa kwenye CEPA**

Kampeni ya CEPA itashawishi na kufanikisha yafuatayo:

1. Mwongozo mpya wa WHO wa HAART, na PMTCT unakubaliwa na serikali na wadau na kutekelezwa nchini kote. Aidha kuhakikisha mwongozo huu unaeleweka kwa watoa huduma za afya.
2. Watoto wanaozaliwa na akina mama wenye VVU wanapima na kupatiwa majibu ndani ya wiki 10. Upatikanaji wa dawa za kuzuia au kutibu VVU zinapatikana pamoja na Seprine..
3. Kutenga fedha ya kutosha kwa ajili ya matumizi ya P M T C T ili kufikia asilimia 80 ya waohitaji huduma hizi kama ilivyo ainishwa katika mkakati wa Wizara ya Afya mwaka 2008 - 2013.